4.5.19 Mapato yasiyotokana na riba yalifikia shilingi milioni 591.15 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na shilingi milioni 572.16 iliyoripotiwa mwaka 2011.

4.5.20 Kwa mwaka 2012 gharama za uendeshaji wa benki ilikuwa ni shilingi millioni 4,154 ikilinganishwa na gharama ya shilingi millioni 2,407 kwa mwaka 2011.

4.5.21 Vigezo muhimu vya utendaji wa benki vilikuwa kama ifuatavyo:

| | | 2012 | 2011 | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| i. | Faida kutokana na mali zote | -1.70% | 00% | -1.70% |
| ii. | Faida kutokana na mtaji | -7.60% | 00% | -7.60% |
| iii. | Mapato yasiyo na riba kwa mapato yaliyo na riba | 13.00% | 19.00% | 6.00% |
| iv. | Gharama kwa mali zote | 10.3% | 7.00% | 3.30% |
| v. | Riba halisi kwa pato la wastani kwa mali zote | 7.5% | 6.00% | 1.50% |
| vi. | Gharama isiyo na riba kwa pato ghafi | 80.7% | 67.00% | 13.70.% |

4.5.22 Fedha taslimu na salio la fedha katika Benki Kuu liliongezeka kwa shilingi millioni 1,122 kulinganisha na mwaka uliopita. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana za benki.

4.5.23 Masalio mengine ya fedha za benki yaliongezeka kwa shilingi milioni 469.1 (26%) ukilinganisha na mwaka uliopita. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa mikopo na benki kuwekeza pesa zake kwenye dhamana za Serikali.

4.5.24 Hali ya uwekezaji katika masoko mengine ya kifedha ilipungua kwa kiwango cha shilingi millioni 1,677 (-18%) ikilinganishwa na mwaka uliopita. Punguzo hilo lilitokana na ongezeko la uwekezaji wa benki kwenye dhamana za Serikali ambazo zilikuwa na riba nzuri kuliko uwekezaji kwenye benki zingine za biashara

4.5.25 Mikopo iliongezeka kwa kiasi cha shilingi millioni 5,139 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Fedha ambazo hazikuwa kwenye mkondo wa kibiashara ziliwekezwa kwenye dhamana za muda mrefu na muda mfupi huku benki ikiimarisha ukopeshaji na usimamizi wa mikopo hiyo.

4.5.26 Mali na vifaa vya benki ziliongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 677.26 (-273%) ikilinganishwa na mwaka uliopita. Ongezeko hilo lilitokana na ununuzi wa mali mpya hasa genereta, kompyuta samani na vifaa vingine vya kuendeshea matawi matatu mapya.

4.5.27 Mali nyingine zilipungua kwa asilimia 7% kutoka mwaka uliopita kufikia kiasi cha shilingi milioni 294.44.

4.5.28 Amana ziliongezeka kwa asilimia 29% kufikia shilingi bilioni 28.30 kutoka shilingi bilioni 21.92 mwaka 2011. Hii ilitokana na juhudi kubwa za kampeni ya uhamasishaji kwa umma ili waweze kuweka fedha zao katika benki yetu.

4.5.29 Madeni mengineyo yalipungua kwa kiasi cha shilingi milioni 100 kutokana na kupungua kwa mikopo kuliko tokana na ulipwaji wa mkopo wa kilimo kwenye benki ya TIB

4.5.30 Akiba isiyogawiwa iliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 187.78. Ongezeko hilo lilitokana na kukua kwa mikopo isiyorejeshwa ambayo kwa mwaka ilikuwa shilingi milioni 653.08. Hali hiyo ndiyo iliyosababisha kupungua kwa mapato ya benki.

4.5.31 Vigezo muhimu vya uwiano wa utendaji wa benki vilikuwa kama inavyoonekana hapa chini:-

**Vigezo muhimu vya uwiano wa utendaji wa benki**

| na | Taarifa | 2012 | 2011 | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| i | Jumla ya mtaji kwa jumla ya mali zote | 23.00% | 27.00% | -4.00% |
| i | Mikopo isiyolipika dhidi ya mikopo yote | 3.90% | 4.60% | -0.70% |
| iii | Mikopo ghafi dhidi ya amana tegemezi zote | 60.00% | 52.00% | 8.00% |
| iv | Mikopo yote dhidi ya mali zote | 42.00% | 34.00% | 8.00% |
| v | Uwiano wa ukwasi | 64.00% | 76.00% | -12.00% |

4.5.32 Bodi ya Wakurugenzi ilithibitisha kuwa benki ilitayarisha taarifa zake za fedha na hesabu kwa kuzingatia dhana ya uendelevu wa shughuli zake. Bodi ya Wakurugenzi ilikuwa na kila sababu ya kutegemea kuwa Benki ya Biashara ya Mkombozi ilikuwa na mali na raslimali za kutosha kuendelea na biashara hiyo na kuendelea kuwepo katika siku za mbele na ilikuwa na ukwasi wa kutosha

4.5.33 Uhusiano kati ya wafanyakazi na menejimenti uliendelea kuwa mzuri. Malalamiko yote yaliyohusu wafanyakazi yalitatuliwa kwenye mikutano na mazungumzo ya kawaida. Benki iliendelea kutoa mafunzo, huduma za afya na mikopo kwa wafanyakazi wake

4.5.34 Benki iliendelea kutoa haki kwa kila mtu katika kupata ajira, kupandishwa vyeo bila upendeleo. Hadi tarehe 31 Desemba, 2012 benki ilikuwa na wafanyakazi kama ilivyoainishwa hapa chini.

| JINSIA | 31 Des 2012 | 31 Des 2011 |
|---|---|---|
| Wanaume | 48 | 18 |
| Wanawake | 33 | 20 |
| **Jumla** | **81** | **38** |

4.5.35 Benki iliangalia kwa makini mtaji timilifu kufuatana na vigezo vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Vigezo hivyo ni kupima mtaji timilifu kwa kulinganisha na mtaji halisi kwa uwiano wa mali katika mizania, ahadi maandishi nje ya mizania na soko, na kwa kulingana na wastani wa tishio la hatari katika siku za mbele.

4.5.36 Mtaji timilifu wa benki kwa vigezo vinavyotakiwa kufikia tarehe 31 Desemba, 2012 ulikuwa kama ifuatavyo:-

| | Kiasi bayana cha waraka mizania mwaka 2012 TZS'000 | Kiasi kilicho hatarini mwaka 2012 TZS'000 | Kiasi bayana cha waraka mizania mwaka 2011 TZS'000 | Kiasi kilicho hatarini mwaka 2011 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| Waraka mizania wa mali **(Mahitaji halisi)** | | | | |
| Fedha taslimu na salio katika Benki Kuu | 5,506,854 | - | 4,384,435 | - |
| Salio kwenye benki zingine (20%) | 2,255,142 | 451,028 | 1,785,976 | 357,195 |
| Hundi na vitu vinavyotarajiwa kukusanywa (50%) | 8,757 | 4,379 | 37,684 | 18,842 |
| Uwekezaji wa fedha kwenye taasisi zingine (20%) | 7,414,028 | 1,482,806 | 9,091,915 | 1,818,383 |
| Mikopo na karadha (100%) | 16,694,000 | 16,694,000 | 11,555,634 | 11,555,634 |
| Dhamana za Serikali | 5,456,269 | - | 5,566,368 | - |
| Uwekezaji kwenye kampuni (100%) | 20,000 | 20,000 | - | - |
| Mali zingine (100%) | 294,448 | 294,448 | 383,035 | 383,035 |
| Kodi iliyoahirishwa (100%) | 349,783 | 349,783 | 391,675 | 391,675 |
| Marekebisho ya pango (100%) | 1,201,830 | 1,201,830 | 149,955 | 149,955 |
| Mali na vifaa (100%) | 925,399 | 925,399 | 248,131 | 248,131 |
| Mali zilizopimilika (100%) | 29,011 | 29,011 | 49,917 | 49,917 |
| **Jumla** | **40,155,521** | **21,452,683** | **33,644,725** | **14,972,767** |
| **Hali ya waraka mizania nje ya salio** | | | | |
| Barua za mikopo zilizopo (20%) | - | - | 202,088 | 40,418 |
| Dhamana na ahadi zilizopo (0%) | | | | |
| | 194,004 | - | 695,610 | - |
| **Jumla ya hali ya waraka mizania nje ya salió** | **194,004** | **-** | **897,698** | **40,418** |
| **Jumla ya mali yote** | **40,349,525** | **21,452,683** | **34,542,423** | **15,013,185** |
| | **Mtaji** | **Uwiano** | **Mtaji** | **Uwiano** |
| **Mtaji wa ngazi ya 1** | **7,241,813** | **33.76%** | **8,484,583** | **56.67%** |
| **Mtaji wa ngazi ya 1 + Mtaji ngazi ya 2** | **7,241,813** | **33.76%** | **8,484,583** | **56.51%** |

4.5.37 Wanahisa walipokea ripoti ya Bodi ya Wakurugenzi na kuijadili. Wanahisa walibaini kwamba vitabu vya mkutano viligawiwa kwa Wanahisa siku ya Mkutano majira ya asubuhi. Hii iliwafanya washindwe kusoma kwa muda mfupi ili waweze kuchangia. Kutokana na hilo Wanahisa waliazimia kwamba vitabu vya mikutano viwepo kwenye matawi ya benki wiki moja kabla ili waweze kuchukua na kusoma mapema kabla ya mkutano.

Annual Riport 2014 Kisw. Output:Layout 1 7/2/14 10:08 AM Page 28

4.5.38 Wanahisa walipokea, walijadili na kuipitisha ripoti ya Wakurugenzi kama ilivyowasilishwa.

## 4.6 KUPOKEA NA KUJADILI RIPOTI YA MKAGUZI WA NJE WA BENKI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2012

4.6.1 Ilitaarifiwa kwamba mkaguzi wa nje wa benki alikuwa ni Ernst & Young ambaye alikagua hesabu za benki na kutoa mchanganuo wa mtiririko wa fedha kwa mwaka 2012 pamoja na kuonyesha kanuni za kiuhasibu.

4.6.2 Ilitaarifiwa kwamba Wakurugenzi wa benki walikuwa na wajibu wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha zinazoeleweka kwa kufuata kanuni za kimataifa za uandishi wa taarifa za fedha na pia kufuata sheria ya makampuni ya mwaka 2002 pamoja na sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006.

4.6.3 Ilitaarifiwa kuwa wajibu wa mkaguzi wa hesabu za benki ni kutoa maoni kuhusu taarifa hizo kwa kufuatana na kazi ya ukaguzi waliyofanya.

4.6.4 Ilitaarifiwa kuwa mkaguzi wa nje alifanya ukaguzi kwa kufuata kanuni za kimataifa za ukaguzi wa taarifa za fedha. Viwango hivyo vilimtaka mkaguzi kufuata kanuni zinazotakiwa na kuandaa mpango wa kufanya ukaguzi ili kujiridhisha kama taarifa hizo za fedha hazina mawaa yanayoweza kuzuia ukweli wa ukaguzi.

4.6.5 Ilitaarifiwa kwamba taarifa za fedha zilizoandaliwa na kukaguliwa zilitoa hali halisi ya kifedha ya benki kufikia tarehe 31 Desemba, 2012 na mwenendo wake ulizingatia kanuni za kimataifa za hesabu, sheria ya kampuni ya Tanzania ya mwaka 2002 na sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006.

4.6.7 Wanahisa walipokea taarifa ya mkaguzi wa nje, walijadili na kuipitisha kama ilivyowasilishwa.

## 4.7 KUPOKEA NA KUJADILI MPANGO WA KUNUNUA HISA KWA HAKI STAHILI KWA WANAHISA KWA AJILI YA KUKUZA MTAJI WA BENKI

4.7.1 Ilitaarifiwa kwamba Benki Kuu ya Tanzania imeongeza kiwango cha chini cha mtaji wa kutoka shilingi bilioni tano hadi shilingi bilioni 15 kwa benki zote za bishara nchini ifikapo mwezi machi, 2015.

4.7.2 Ilitaariwa kwamba ongezeko hilo la mtaji wa benki lilitolewa kwenye gazeti la Serikali namba 68 la mwaka 2012 lililochapishwa tarehe 2 Machi, 2012 ambalo lilizitaka benki zote za biashara nchini kuwa na kima cha chini cha mtaji cha shilingi bilioni 15 ifikapo mwezi Machi, 2015.

4.7.3 Ilitaarifiwa kwamba benki zote za biashara ambazo zilikuwa hazijatimiza mtaji wa shilingi bilioni kumi na tano zililipewa kipindi cha msamaha cha miaka mitatu toka tarehe ya tangazo la serikali.

4.7.4 Ilitaarifiwa kwamba kipindi cha msamaha huo kitaisha mwezi Machi, 2015. Kutokana na sababu hii Bodi ya Wakuruigenzi pamoja na Menejimenti iliwaomba Wanahisa kupitisha azimio la kununua hisa kwa mpango wa hisa stahili kwa uwiano wa 1:1. Hii ilimainisha kwamba kama Mwanahisa anamiliki hisa 100 anaweza kuongeza tena hisa nyingine 100.

4.7.5 Wanahisa walijadili mpango huo na hatimaye walipitisha azimio lifuatalo:

Katika Mkutano Mkuu wa Nne wa Wanahisa uliofanyika tarehe 25, Mei, 2013 Wanahisa wa benki ya biashara ya Mkombozi walikubaliana na kuridhia mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya kuongeza mtaji wa benki kwa mpango wa hisa stahili kwa kila Mwanahisa kununua hisa kwa uwiano wa 1:1. Wanahisa waliitaka Bodi ya Wakurugenzi kuchukua juhudi zote za kufuata kanuni za uuzaji wa hisa hizo na endapo Mwanahisa atashindwa kununua hisa anazostahili, Mwanahisa mwingine wa benki atakuwa huru kuzinunua.

## 4.8 KUTEUA MKAGUZI WA NJE WA BENKI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA 2013

4.8.1 Ilitaarifiwa kwamba kifungu namba 5(1) cha kanuni za wakaguzi wa nje wa benki za bishara kinaeleza kwamba kila benki itateua mkaguzi wa nje ambaye atachaguliwa kila mwaka ambaye hatakuwa na maslahi na benki na kuitaarifu Benki Kuu jina la mkaguzi huyo.

4.8.2 Ilitaarifiwa kwamba kifungu namba 5(4) cha kanuni za wakaguzi wa nje wa benki za bishara kinaeleza kwamba mkaguzi wa nje wa benki haruhusiwi kukagua benki hiyo hiyo kwa kipindi kinachozidi miaka minne

4.8.3 Ilitaarifiwa kwamba ERNST & YOUNG walikuwa wakaguzi wa nje kwa kipindi cha miaka minne na kwa misingi ya kifungu hicho hawakuwa na sifa ya kuchaguliwa tena.

4.8.4 Ilitaarifiwa kwamba Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya benki ilikaribisha maombi kwa kampuni sita ambazo zinazoruhusiwa na Benki Kuu kufanya ukaguzi wa hesabu za benki kwenye benki za biashara nchini ili zitoe mapendekezo ya gharama zao kufanya kazi ya kukagua hesabu za benki kwa mwaka 2013.

4.8.5 Katika kampuni sita ni kampuni nne tu zilionyesha nia ya kufanya kazi ya ukaguzi wa fedha. Majina ya kampuni hizo na sifa zao ziliorozeshwa kama inavyoonekana hapa chini.

| JINA | KIWANGO BEI | SIFA YA UKAGUZI KWENYE BENKI ZA BIASHARA |
|---|---|---|
| 1. PRICEWATERHOUSECOOPERS | Dola 22,000 kabla ya VAT | 14 |
| 2. DELOITTE & TOUCHE | Dola 27,000 kabla ya VAT | 7 |
| 3. TAC ASSOCIATES | Shilingi 35,907,400 pamoja na VAT ya shilingi 5,477,400 | 1 |
| 4. PKF TANZANIA | Dola 12,900,000 kabla ya VAT | Hakuna |

4.8.6 Ilitaarifiwa kuwa Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza kampuni ya PriceWaterHouseCoopers (PWC) kukagua hesabu za benki kwa mwaka 2013 kwa gharama ya dola za Marekani 20,000 kabla ya kodi ya ongezeka la thamani badala ya Dola 22,000.00 kabla ya kodi ya ongezeka la thamani.

4.8.7 Bodi ya Wakurugenzi iliwaomba Wanahisa kuipitisha kampuni ya PriceWaterHouseCoopers (PWC) kukagua hesabu za benki kwa mwaka 2013 kwa gharama ya dola za Marekani 20,000 kabla ya kodi ya ongezeka la thamani.

4.8.8 Wanahisa kwa pamoja walikubali kuipatia kampuni ya PriceWaterHouseCoopers (PWC) kazi ya kukagua hesabu za benki kwa gharama ya Dola za Kimarekani 20,000 kabla ya kodi ya ongezeka la thamani.

## 4.9 KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA WANAHISA KWA MWAKA 2014

Wanahisa kwa pamoja walikubaliana kuwa Mkutano Mkuu utakaofuata ufanyike Jumamosi ya mwisho ya mwezi Mei, 2014 ambayo itakuwa tarehe 31, Mei, 2014.

## 4.10 KUJADILI MENGINEYO KWA RUHUSA YA MWENYEKITI

4.10.1 Wanahisa walibaini kuwa taarifa kati ya benki na Wanahisa hazikuwa zikiwafikia wao kama inavyotakiwa. Bodi ya Wakurugenzi iliripoti kuwa taarifa mbalimbali za benki zinapatikana kwenye tovuti ya benki na Bodi iliwaomba Wanahisa kuangalia kwenye tovuti hiyo mara kwa mara. Kuhusu taarifa ya mkutano Bodi ilitoa taarifa kuwa benki ilituma ujumbe wa mkutano kwa kila Mwanahisa kwenye simu yake ya mkononi.

4.10.2 Wanahisa walitaka kujua ni lini benki itajiorodhesha kwenye soko la hisa. Bodi ya Wakurugenzi iliripoti kuwa kwa muda huo benki haikuwa na uwezo wa kujiunga kwenye soko la hisa badala yake ilipendekeza kukuza mtaji kwa njia ya ununuzi wa hisa kwa haki stahili kwa kila Mwanahisa.

4.10.3 Wanahisa walibaini kuwa benki ilikuwa haijitangazi vya kutosha ukilinganisha na benki zingine. Bodi ya Wakurugenzi iliripoti kuwa matangazo kwenye vyombo vya habari ni gharama kubwa sana. Hata hivyo benki ilitoa matangazo mengi sana kwenye vyombo mbalimbali vya habari na inawezakana baadhi ya Wanahisa hawakuweza kuyasikia matangazo hayo kwa sababu vyombo vya habari ni vingi mno.

**4.11 KUFUNGA MKUTANO**

Mwenyekiti alifunga mkutano saa 9 alasiri.

Imetolewa tarehe leo……….Mwezi wa ……………mwaka 2014

| | |
|---|---|
| ____________________ | ____________________ |
| MASHA JOHN MSHOMBA | BALTAZAR BALTAZAR MBILINYI |
| **MWENYEKITI WA BODI** | **KATIBU WA BODI** |

## 5.4 YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA NNE WA MWAKA WA WANAHISA ULIOFANYIKA TAREHE 25 MEI, 2013

| Kumb.Na. | MAELEKEZO | MATOKEO |
|---|---|---|
| 4.6.3 | Wanahisa walipokea ripoti ya Bodi ya Wakurugenzi na kuijadili. Wanahisa walibaini kwamba vitabu vya mkutano viligawiwa kwa Wanahisa siku ya Mkutano majira ya asubuhi. Hii iliwafanya washindwe kusoma kwa muda mfupi ili waweze kuchangia. Kutokana na hilo Wanahisa waliazimia kwamba vitabu vya mikutano viwepo kwenye matawi ya benki wiki moja kabla ili waweze kuchukua na kusoma mapema kabla ya mkutano. | Hili limetekelezwa. Vitabu kwa ajili ya mkutano vilisambazwa kwenye matawi ya benki wiki moja kabla ya Mkutano |
| 4.7.5 | Wanahisa walijadili mpango huo na hatimaye walipitisha azimio lifuatalo:<br>Katika Mkutano Mkuu wa Nne wa Wanahisa uliofanyika tarehe 25, Mei, 2013 Wanahisa wa benki ya biashara ya Mkombozi walikubaliana na kuridhia mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya kuongeza mtaji wa benki kwa mpango wa hisa stahili kwa kila Mwanahisa kununua hisa kwa uwiano wa 1:1. Wanahisa waliitaka Bodi ya Wakurugenzi kuchukua juhudi zote za kufuata kanuni za uuzaji wa hisa hizo na endapo Mwanahisa atashindwa kununua hisa anazostahili, Mwanahisa mwingine wa benki atakuwa huru kuzinunua. | Agizo hili lilitekelezwa kuanzia tarehe 25 Novemba, 2013 na kwisha tarehe 28 Februari, 2014 na baadaye kupata muda nyongeza hadi tarehe 14 Machi, 2014. Katika zoezi hili benki iliweza kukusanya shilingi 5,819,383,600.10 |
| 4.8.8 | Wanahisa kwa pamoja walikubali kuipatia kampuni ya PriceWaterHouseCoopers (PWC) kazi ya kukagua hesabu za benki kwa gharama ya Dola za Kimarekani 20,000 kabla ya kodi ya ongezeka la thamani.<br>Coopers (PWC) kuwa<br>na | Hili lilitekelezwa. Tarehe 30 Mei Menejimenti ya benki iliwataarifu Price Water House wamechaguliwa Wanahisa kuwa |

| Kumb.Na. | MAELEKEZO | MATOKEO |
|---|---|---|
| | | wakaguzi wa nje wa benki kwa mwaka, 2013. Tarehe 3 Julai. Price Water House Coopers (PWC walikubali mwito huo. wamefanya ukaguzi wa hesabu za benki kwa kipindi cha mwaka 2013 na watawasilisha taarifa yao kwenu ninyi Wanahisa. |
| 4.9 | Wanahisa kwa pamoja walikubaliana kuwa Mkutano Mkuu utakaofuata ufanyike Jumamosi ya mwisho ya mwezi Mei, 2014 ambayo itakuwa tarehe 31, Mei, 2014.<br>tarehe 31 Mei, 2014 | Agizo hili limetekelezwa Mkutano Mkuu wa Tano unafanyika leo ikiwa ni Jumamosi ya mwisho ya mwezi wa tano. |
| 4.10.2 | Wanahisa walitaka kujua ni lini benki itajiorodhesha kwenye soko la hisa. Bodi ya Wakurugenzi iliripoti kuwa kwa muda huo benki haikuwa na uwezo wa kujiunga kwenye soko la hisa badala yake ilipendekeza kukuza mtaji kwa njia ya ununuzi wa hisa kwa haki stahili kwa kila Mwanahisa. | Hoja hii ipo kwenye ajenda namba sita kwenye mkutano huu ambayo itajadiliwa kw kina |
| 4.10.3 | Wanahisa walibaini kuwa benki ilikuwa haijitangazi vya kutosha ukilinganisha na benki zingine. Bodi ya Wakurugenzi iliripoti kuwa matangazo kwenye vyombo vya habari ni gharama kubwa sana. Hata hivyo benki ilitoa matangazo mengi sana kwenye vyombo mbalimbali vya habari na inawezakana baadhi ya Wanahisa hawakuweza kuyasikia matangazo hayo kwa sababu vyombo vya habari ni vingi mno. | Benki inaendelea kujitangaza wakati wote kupitia vyombo mbalimbali vya matangazo. |

## 5.5 TAARIFA YA BODI YA WAKURUGENZI WA BENKI KWA MWAKA 2013

### 5.5.1 Taarifa ya Mwenyekiti wa Bodi

#### 5.5.1.1 Utangulizi

Wapendwa Wanahisa, Mabibi na Mabwana habari za asubuhi;
Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mkombozi, nachukua fursa hii kuwakaribisha kwenye Mkutano Mkuu wa tano wa benki yetu. Mtakumbuka kwamba tulikutana kwenye Mkutano Mkuu wa nne uliofanyika tarehe 25 Mei, 2013 katika ukumbi huu na tuliripoti, pamoja na mambo mengine, juu ya utendaji wa benki kwa kipindi cha mwaka 2012. Leo tena kama ilivyo wajibu wetu wa kutoa taarifa, tutatoa ripoti ya benki kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2013. Pamoja nasi, kuna Mkaguzi wa nje wa hesabu za benki ambaye aliteuliwa kwenye mkutano wetu wa mwaka jana uliofanyika tarehe 25 Mei 2013.

#### 5.5.1.2 Mikakati ya benki kwa mwaka 2013

Kwa kipindi cha mwaka 2013 benki ilipanga kutekeleza malengo kadhaa ikiwa ni pamoja na ukuaji wa rasilimali za benki hadi kufikia shilingi bilioni 77.03. Mkurugenzi Mtendaji atatoa taarifa kwenu juu ya mafanikio ya malengo haya.

#### 5.5.1.3 Kukuza mtaji

Mtaji ulioidhinishwa wa benki ni shilingi bilioni 50.00 Mwaka jana tuliwataarifu kwamba Benki Kuu ilitoa tangazo la Serikali la kuongeza mtaji wa benki kwa benki zote za biashara nchini kufikia kima cha chini cha shilingi bilioni 15.00, ifikapo tarehe 31 Machi 2015. Kutokana na hilo, ninyi Wanahisa mlipitisha azimio la kuongeza mtaji wa benki kupitia uuzaji wa hisa za benki kwa Wanahisa wote kwa njia ya hisa stahili. Pia mlisisitiza na kuielekeza Bodi na Menejimenti ya benki kutekeleza mpango wa uuzaji wa hisa za benki kwa njia ya hisa stahili. Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa benki, napenda kuwataarifu kuwa uuzaji wa hisa za benki kwa Wanahisa wake kwa mpango wa hisa stahili ulitekelezwa kama mlivyotuelekeza. Matokeo ya mpango huu yatawasilishwa kwenu kwenye ajenda ya yatokanayo ambayo ni moja kati ya ajenda za mkutano huu. Pamoja na hayo kwa msisitizo tunawataarifu kuwa mpango wa uuzaji wa hisa kwa wanahisa wake ulifunguliwa mnamo tarehe 25 Novemba 2013 na kufungwa rasmi

tarehe 14 Machi, 2014. Katika zoezi hili benki iliweza kukusanya shilingi bilioni 5.82 kutoka kwa Wanahisa wake ikiwa ni mauzo ya hisa stahili kwa Wanahisa walioshiriki. Nachukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru wote walioshiriki kununua hisa za benki.

**5.5.1.4 Mpango wa kujiunga na Soko la Hisa la Dar es salaam.**

Wapendwa Wanahisa mtakumbuka kwamba tarehe 6 Mach, 2007 benki hii ilisajiliwa kama benki binafsi. Ilipofika tarehe 29 Septemba, 2010 benki hii ilibadilika kutoka kampuni binafsi na kuwa kampuni au benki ya watu wengi yaani kuwa ya umma. Sababu kubwa ya badiliko hilo ilikuwa ni kutimiza matakwa ya sheria za nchi.

Ili kukuza mtaji wake benki iliomba ruhusa kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji nchini kuwauzia Wanahisa wake hisa kwa njia ya hisa stahili kama ilivyoazimiwa na Wanahisa kwenye Mkutano Mkuu wa Nne uliofanyika tarehe 25 Mei, 2013. Katika zoezi hili benki ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 5.82. Hata hivyo, pamoja na mafanikio haya yaliyopatikana kupitia uuzaji wa hisa kwa njia ya hisa stahili, benki bado haitaweza kutimiza maelekezo ya Benki Kuu baada ya kuongeza mtaji huo. Hii ni kwa sababu zoezi la uuzaji wa hisa kwa njia ya hisa stahili limeongeza mtaji wa benki (core capital) hadi kufikia kufikia shilingi bilioni 14.00 tu wakati maelekezo ya Benki Kuu ni kuwa na mtaji wa chini wa shilingi bilioni 15.00 ifikapo Machi, 2015.

Kutokana na sababu hii, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya benki inapendekeza ajenda maalumu kwa Wanahisa kupitisha azimio litakalo iwezesha benki kujiunga na Soko la Hisa la Dar es salaam na kuuza hisa 5,000,000 kwa umma. Kujiunga kwenye Soko la Hisa la Dar es salaam kuna faida mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza mtaji wa benki na hivyo kutimiza taratibu za kisheria zilizowekwa na Benki Kuu ya Tanzania, kufungua matawi mapya na kuanzisha wakala wa benki.

**5.5.1.5 Mipango ya benki kwa mwaka 2014**

Katika mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba, 2014 benki ina mpango wa kutekeleza mipango ifuatayo:

(i) Kukuza mtaji wa benki;

(ii) Kuendelea kutoa mikopo kwa wateja wakubwa, wa kati na wadogo;

(iii) Kuongeza amana za benki;
(iv) Kufungua matawi mawili;
(v) Kuanzisha huduma za uwakala wa benki; na
(vi) Kukuza rasilimali za benki.

Mwelekeo wa utendaji wa benki kwa mwaka huu ni mzuri. Kwa kipindi cha miezi mitatu kuishia tarehe 31 Machi, 2014 benki imepata faida ya Tsh 565 milioni. Hesabu hizi hazijakaguliwa lakini zimetangazwa kwenye magazeti.

**5.5.1.5 Utendaji wa benki kwa mwaka 2013**

Benki ilipata faida ya shilingi milioni 119.01 kwaka 2013. Mkurugenzi Mtendaji atatoa taarifa juu ya utendaji wa benki kwa kina zaidi kwa mwaka 2013.

**5.5.1.6 Wanahisa**

Vitabu ambavyo tumevigawa vinaonyesha mtiririko na maelezo yote ya hesabu za benki kwa kipindi chote cha mwaka 2013. Wakaguzi wetu wa nje wa hesabu za benki watatoa taarifa yao kwa ajili ya majadiliano. Mapendekezo, maoni na mchango wenu katika ajenda hii ni muhimu sana ili kuiendesha benki hii kwa ufanisi. Nawaomba msome taarifa hiyo na msisite kuuliza maswali kwa ufafanuzi zaidi. Baada ya kusema hayo naomba nimkaribishe Mkurugenzi Mtendaji Bibi Edwina Agnellus Lupembe ili aweze kuwapa taarifa ya utendaji wa benki kwa kina zaidi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Nawasilisha

**MWENYEKITI WA BODI**
**31 MEI 2014**

### 5.5.2 Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji

#### 5.5.2.1 Utangulizi

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, pamoja na menejimenti ya benki, nachukua fursa hii kuelezea utendaji wa benki ya Mkombozi kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2013. Maelezo ya kina zaidi yapo kwenye vitabu vya mkutano ambavyo tayari tumekwisha wagawia. Kama Mwenyekiti alivyosema, tafadhali someni vitabu hivyo na iwapo kuna maswali msisite kuuliza maana tupo hapa kwa ajili yenu ili kuendesha benki hii kwa pamoja.

#### 5.5.2.2 Malengo makuu ya benki kwa mwaka 2013

(i) Kukuza mtaji wa benki kufikia shilingi bilioni 17.00;
(ii) Kuendelea kutoa mikopo midogomidogo kufikia shilingi bilioni 3.01;
(iii) Kuendelea kutoa mikopo mikubwa kufikia shilingi bilioni 32.58;
(iv) Kuendelea kutoa mikopo ya wafanyakazi kufikia shilingi bilioni 5.90;
(v) Kuongeza amana kufikia shilingi bilioni 57.32;
(vi) Kuhakikisha kuwa mikopo inarejeshwa kwa asilimia isiyopungua 97;
(vii) Kuendelea kutoa mikopo ya kilimo
(viii) Kukuza rasilimali za benki kufika shilingi 77.03
(ix) Kuzalisha faida ya shilingi milioni 509.16

Malengo haya yaliangaliwa upya kutokana na sababu zifuatazo:

(i) Bajeti nzima ya benki ilitarajiwa kuwa mtaji wa benki ungekuwa umefikia shilingi bilioni 17.00 kufikia mwishoni mwa mwaka. Ilipofika Novemba, 2013 mtaji wa benki ulikuwa ni shilingi bilioni 11.01 tu na hivyo kuwa na uwezo mdogo wa uwekezaji katika dhamana za Serikali.
(ii) Bajeti ya benki kwa mwaka 2013 ilidhamiria kuwa na mkopo wa fedha za kilimo shilingi bilioni moja kutoka Serikalini na ilipofika Novemba 2013 mkopo huo haukupatikana.
(iii) Mikopo ya benki ilitarajiwa kufikia shilingi bilioni 43.49 ikijumlishwa na mikopo ya kilimo. Malengo hayo yalilenga utendaji mzuri wa matawi mapya matatu. Hata hivyo matawi hayo matatu hayakufikia malengo kwa vile yalifunguliwa mwaka 2012 na hivyo kuwa mapya sokoni.

**5.5.2.3 Malengo mapya yalikuwa kama ifuatavyo:-**

(i) Kukuza mtaji wa benki kufikia shilingi bilioni 17.00
(ii) Kukuza mikopo kufikia shilingi bilioni 32.29;
(iii) Kukuza amana kufikia shilingi bilioni 50.31 ;
(iv) Kukusanya mikopo yote kwa asilimia isiyopungua 97 ;
(v) Kuongeza rasilimali za benki kufikia bilioni 66.95 ; na
(vi) Kuwa na faida ya shilingi milioni 94.18

Ili kukidhi na kutekeleza malengo hayo benki kwa kipindi cha mwaka 2013 ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwatembelea watu binafsi, vikundi, makampuni binafsi na taasisi za mbalimbali ili kuhamasisha kununua hisa za benki;
(ii) Kuwatembelea watu binafsi, makampuni binafisi na taasisi mbalimbali ili kuhamasisha kuweka amana za benki;
(iii) Kuboresha vikundi vidogo vidogo na kuanzisha vipya kwa ajili ya kuendelea kutoa mikopo midogo midogo kwa wateja wetu;
(iv) Kuendelea kutoa mikopo kwa wafanyakazi;
(v) Kuandaa mazingira mazuri ya ajira binafsi kwa wateja kwa kutoa elimu ya ujasiriamali;
(vi) Kutoa mikopo ya kilimo; na
(vii) Kuanzisha huduma mpya za benki kwa njia ya simu

**5.5.2.3 Mafanikio ya benki kwa mwaka 2013**

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2013 mafanikio ya benki yalikuwa kama ifuatavyo:-

**5.5.2.4 Amana**

Benki iliweza kukusanya amana za shilingi bilioni 49.78 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 50.31.

**5.5.2.5. Mikopo na karadha**

Napenda kutoa tarifa kuwa mikopo yote hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2013 ilifikia shilingi bilioni 28.88 ukilinganisha na malengo ya shilingi bilioni 32.29. Mwaka 2012 benki ilitoa mikopo kufikia shilingi bilioni 16.69

**5.5.2.6 Matokeo ya uendeshaji wa benki kwa mwaka 2013**

Benki ilipata mapato yatokanayo na riba ya shilingi bilioni 4.74 ukilinganisha na riba ya shilingi bilioni TZS 2.88 iliyoripotiwa mwaka 2012 na iliingia gharama ya riba ya shilingi bilioni 2.36. Benki pia ilipata mapato yasiyotokana na riba ya shilingi milioni 850.27 ikilinganishwa na shilingi milioni 591.11 iliyoripatikana mwaka 2012.

**5.5.2.7 Gharama za uendeshaji wa benki kwa mwaka 2013**

Jumla ya gharama zote za uendeshaji wa benki kwa kipindi cha mwaka 2013 ilikuwa ni shilingi bilioni 5.24 ukilinganisha na shilingi bilioni 4.15 kwa mwaka 2012. Ongezeko la gharama za uendeshaji limetokana na ongezeko la biashara na zoezi la uuzaji wa hisa kwa njia ya hisa stahili.

**5.5.2.8 Rasilimali za benki**

Jumla ya rasilimali za benki zilifikia shilingi bilioni 64.02 ikilinganishwa na shilingi bilioni 40.15 iliyoripatikana mwaka 2012

**5.5.2.9 Faida kwa mwaka**

Benki ilipata faida( kabla ya kodi) ya shilingi milioni 342.67 na ilipata gharama ya kodi ya shilingi milioni 223.65 na kupata faida halisi ya shilingi milioni 119.01 ikilinganishwa na mwaka 2012 ambapo benki ilipata hasara ya shilingi milioni 716.70.

**5.5.2.10 Ajira**

Jumla ya idadi ya wafanyakazi wote kufikia tarehe 31 Desemba 2013 ilikuwa ni 86; ukilinganisha na wafanyakazi 81 mwaka 2012. Hii inajumuisha wanaume 52 na wanawake 34.

Nawasilisha.

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**31 MEI 2014**

## 5.6 KAZI YA BENKI

Kazi ya benki ilikuwa ni kutoa huduma za benki na masuala yote yahusuyo benki kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006. Hapakuwa na mabadiliko yeyote kuhusu kazi hizo kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2013.

## 5.7 MTAJI WA BENKI

Mtaji wa benki hadi hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2013 ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini.:-

**Mtaji uliohidhinishwa**

Hisa 50,000,000 za kawaida zenye thamani ya shilingi 1000 kila hisa.

**Hisa zilizolipwa**

Hisa 11,013,784 za kawaida zenye thamani ya shilingi 1000 kila hisa.

## 5.7 MGAWANYO WA WANAHISA WA BENKI.

Jumla ya hisa zote zilizolipiwa hadi mwishoni mwa mwaka 2013 ilikuwa ni 11,013,784 (Mwaka 2012: ilikuwa ni hisa 11,013,784 )
Mgawanyiko wa hisa ni kama ifutavyo:

| JINA | IDADI YA HISA | THAMANI (TZS) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Majimbo na Taasisi zake | 2,973,722 | 2,973,722,000 | 27% |
| Taasisi mbalimbali | 1,762,205 | 1,762,205,000 | 16% |
| Baraza la Maaskofu | 2,643,308 | 2,643,308,000 | 24% |
| Watu binafsi | 3,634,549 | 3,634,546,000 | 33% |
| **Jumla** | **11,013,784** | **11,013,784,000** | **100%** |

Jumla ya hisa mwishoni mwa mwaka 2012 ilikuwa hisa 11,013,784 kama ifuatavyo:

| JINA | IDADI YA HISA | THAMANI (TZS) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Majimbo na Taasisi zake | 2,973,722 | 2,973,722,000 | 27% |
| Taasisi mbalimbali | 1,762,205 | 1,762,205,000 | 16% |
| Baraza la Maaskofu | 2,643,308 | 2,643,308,000 | 24% |
| Watu binafsi | 3,634,549 | 3,634,546,000 | 33% |
| **Jumla** | **11,013,784** | **11,013,784,000** | **100%** |

## 5.8 WAKURUGENZI WA BENKI

Wakurugenzi wa benki ambao walitumikia benki kwa kipindi chote cha mwaka 2013 ni kama ifuatavyo.

| Jina | Wadhifa | Tarehe ya kuzaliwa | Wasifu/ Ujuzi | Uraia | Tarehe ya uteuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Bw. Masha John Mshomba | Mwenyekiti | 8 Mei, 1971 | Shahada ya Uzamili katika masuala ya fedha, CPA na Shahada ya Uzamili katika biashara za kimataifa, (Mkurugenzi wa fedha na utawala PSPF) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18,2009 |
| Bw Method Anatoli Kashonda | Naibu Mwenyekiti | 15 Februari 1945 | Shahada ya Uzamili katika masuala ya fedha, (MBA)FCCA, FCPA (Mbia mwandamizi Globe Accountancy Services) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |
| Bibi Edwina Agnellus Lupembe | Mkurugenzi Mtendaji | 20 Mei, 1947 | Shahada ya Uzamili katika maswala ya Biashara (MBA) (Mkurugenzi Mtendaji MKCB) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |
| Dkt Eve Hawa Sinare | Mkurugenzi | 26 Juni, 1951 | Shahada ya Uzamivu katika maswala ya Sheria; Wakili na mtaalam Mshauri wa Sheria za biashara na benki (Mshirika Mwandamizi Rex Attonery) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |
| Padre Dkt. Anthony Makunde | Mkurugenzi | 17 Januari 1963 | Shahada ya uzamivu katika maswala ya Theologia (Padre na Katibu Mkuu TEC) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |

| Jina | Wadhifa | Tarehe ya kuzaliwa | Wasifu/ Ujuzi | Uraia | Tarehe ya uteuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Askofu Beatus Kinyaiya | Mkurugenzi | 8 Mei, 1956 | Shahada ya Uzamili (MA) katika Historia, (BA) katika Jiografia (BA) katika Theolojia ya Kiroho (Askofu Jimbo la Mbulu) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |
| Bw Placidus Luoga** | Mkurugenzi | 7 Januari, 1954 | Shahada ya Uzamili katika maswala ya kodi (Mshauri binafsi wa kodi) | Mtanzania | Alijihuzuru Agosti 31, 2013 |
| Mr. Marcellino Kayombo | Mkurugenzi | 3 Agosti 1947 | Stashahada ya juu katika masuala ya Fedha (Afisa wa Benki Mstaafu) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |
| Profesa Marcellina Mvula Chijoriga * | Mkurugenzi | 1 January, 1955 | Shahada ya mzamili katika masuala ya fedha na shahada ya uzamivu katika uchumi. (Profesa wa Chuo Kikuu Cha Dar es salaam kwenye Shule ya Biashara aliyebobea katika masuala ya uchumi na fedha). | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 31, 2013. |
| Baltazar Baltazar Mbilinyi | Mwanasheria na Katibu wa Bodi | 10 Oktoba, 1973 | Shahada ya kwanza ya Sheria (LLB), Shahada ya pili ya sheria (LLM) Wakili na mtaalamu wa sheria za benki na makampuni. (Katibu wa Bodi) | Mtanzania | Aliteuliwa Agosti 18, 2009 |

* Mkurugenzi mpya aliyechukua nafasi ya Bw. Placidus Luoga**

## 5.9 HISA ZA WAKURUGENZI

| JINA | IDADI YA HISA 2013 | IDADI YA HISA 2012 |
|---|---|---|
| Bw. Masha John Mshomba | **5,000** | 5,000 |
| Bw. Method Anatoli Kashonda | **1,000** | 1,000 |
| Bi. Edwina Agnellus Lupembe | **3,500** | 3,500 |
| Dkt. Eve Hawa Sinare | **10,000** | 10,000 |
| Padre Dkt. Antony Makunde | **-** | - |
| Mhashamu Askofu Beatus Kinyaiya | **12,015** | 12,015 |
| Prof.Marcellina Mvula Chijoriga | **-** | - |
| Bw. Placidus Luoga | **1,000** | 1,000 |
| Bw. Marcellino Kayombo. | **1,161** | 1,161 |
| **Idadi ya hisa za Wakurugenzi** | **33,676** | **33,676** |

Hakuna Mkurugenzi anayemiliki hisa zaidi ya asilimia 0.3% ya hisa zote zilizolipwa.

## 5.10 KATIBU WA BENKI

Katibu wa benki mpaka tarehe 31 Desemba 2013 alikuwa ni Bw Baltazar B. Mbilinyi

## 5.11 UTAWALA WA BENKI

Wakurugenzi wamedhamiria kujikita katika misingi ya kuendesha benki kwa kufuata misingi ya utawala bora na wanatambua hitaji la kuendesha shughuli za kibenki kwa kufuata misingi ya utendeaji bora wa kazi.

Bodi ya Wakurugenzi walikutana mara kwa mara kipindi chote cha mwaka. Walikutana ili kuisimamia benki kwa usahihi na kusimamia uendeshaji wa benki.

Kwa kipindi chote cha mwaka 2013 Bodi ilikutana mara 4 katika mikutano yake ya kawaida na ilikutana mara 10 kwenye mikutano ya dharura. Mahudhuria ya wajumbe wa Bodi kwenye mikutano hiyo ni kama ifuatavyo:-

**Mikutano ya Bodi**

| Na | JINA | WADHIFA | IDADI YA MIKUTANO | IDADI YA MIKUTANO ALIYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Masha John Mshomba | Mwenyekiti | 15 | 11 |
| 2. | Bw. Method Anatoli Kashonda | Makamu Mwenyekiti | 15 | 14 |
| 3. | Bi. Edwina Lupembe | Mkurugenzi Mtendaji | 15 | 14 |
| 4. | Dkt. Eve Hawa Sinare | Mkurugenzi | 15 | 8 |
| 5. | Padre Dkt. Antony Makunde | Mkurugenzi | 15 | 13 |
| 6. | Mhashamu Askofu Beatus Kinyaiya | Mkurugenzi | 15 | 7 |
| 7. | Prof.Marcellina Mvula Chijoriga* | Mkurugenzi | 6 | 3 |
| 8. | Bw. Placidus Luoga** | Mkurugenzi | 9 | 9 |
| 9. | Bw. Marcellino Kayombo | Mkurugenzi | 15 | 14 |

*Inahusu miezi 4 tangu alipoteuliwa Agosti 31, 2013.
**Inahusu miezi 8 mpaka alipojiudhuru August 31, 2013

Kila kamati ya Bodi ina mwongozo unaoonyesha kazi na majukumu yanayoonyesha ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Bodi.

**Kamati ya Bodi ya Ukaguzi**

Kamati hii ina jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa sheria na kanuni zilizoidhinishwa kutumika na matakwa ya mamlaka za udhibiti zinazohusika; kupitia taarifa mbalimbali za hesabu za fedha na utendaji; kufuatilia kujibiwa hoja za wakaguzi na utekelezaji wa mapendekezo ya wakaguzi wa nje, wakaguzi wa ndani na wa Benki Kuu ya Tanzania kuhusu tarifa za fedha na uendeshaji wa shughuli za benki.

Wajumbe wa Kamati ya Bodi ya ukaguzi wa hesabu waliotumikia kamati hiyo kwa mwaka 2013 na wasifu wao ni kama ifuatavyo:-

**Kamati ya Ukaguzi**

| Na | JINA | WADHIFA | JUMLA YA MIKUTANO | IDADI YA MIKUTANO ALIYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mr. Method Anatoli Kashonda | Mwenyekiti | 5 | 4 |
| 2 | RT. Rev. Bishop Beatus Kinyaiya | Mkurugenzi | 5 | 5 |
| 3 | Mr. Placidus Luoga | Mkurugenzi | 3 | 2 |
| 4 | Prof.Marcellina Mvula Chijoriga * | Mkurugenzi | 2 | 1 |

*Inahusu miezi 4 tangu alipoteuliwa Agosti 31, 2013.

**Kamati ya Mikopo, Uhatarishi na Ukubalifu**

Kamati hii ilikuwa na jukumu la kuidhinisha na kudhibiti mikopo, kudhibiti vihatarishi katika uendeshaji wa benki na kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni zilizowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Wajumbe waliotumikia Kamati hii kwa kipindi cha mwaka 2013 ni kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA | WADHIFA | IDADI YA MIKUTANO | IDADI YA MIKUTANO ALIYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bw. Marcellino Kayombo. | Mwenyekiti | 13 | 12 |
| 2 | Dkt. Eve Hawa Sinare | Mkurugenzi | 13 | 9 |
| 3 | Padre Dkt. Antony Makunde | Mkurugenzi | 13 | 11 |

## 5.12 MENEJIMENTI

Kwa kipindi cha mwaka 2013 Menejimenti ya benki ilikuwa chini ya Mkurugenzi Mtendaji akisaidiwa na Wakurugenzi wafuatao:-

- Mkurugenzi wa Fedha na Utawala;
- Mkurugenzi wa Uendeshaji wa benki;
- Mkurugenzi wa Hazina;
- Mkurugenzi wa Mikopo;
- Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani;
- Mkurugenzi wa Teknohama; na
- Mkurugenzi wa Huduma za Sheria (Katibu wa Benki)

## 5.13 MAFANIKIO YA BENKI

Benki ilipata faida ya shilingi milioni 342.67 hadi kufika tarehe 31 Desemba, 2013 kabla ya kodi (Mwaka 2012: benki ilipata hasara ya shilingi milioni 716.70 ). Faida baada ya kodi ilikuwa shilingi milioni 119.01 Pamoja na hayo mafanikio yafuatayo yalipatikana:

Mikopo ilifikia shilingi bilioni 28.88 (Mwaka 2012: ilifika shilingi bilioni 16.69);
Jumla ya amana ilikuwa ni shilingi bilioni 49.78 (Mwaka 2012: amana zilikuwa shilingi bilioni 28.30 billion); na Jumla ya rasilimali zilikuwa shilingi bilioni 64.02 ( Mwaka 2012 zilikuwa shilingi bilioni 40.15)

**Matawi ya benki**

Benki ilikuwa na matawi manne hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2013. Matawi matatu yapo Dar es Salaam na moja jijini Mwanza . Idadi ya wateja na wakopaji ilikuwa kama ifuatavyo:

| | **2013** | 2012 |
|---|---|---|
| **Aina ya Akaunti** | | |
| Akaunti za hundi | **774** | 581 |
| Akaunti za akiba | **17,466** | 14,185 |
| Akaunti za muda maalumu | **333** | 132 |
| **Jumla** | **18,573** | 14,898 |
| **Akaunti za mikopo** | **5,875** | 4,877 |

## 5.14 GAWIO

Wakurugenzi wa Bodi hawapendekezi kulipa gawio kwa Wanahisa kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2013.

## 5.15 MIPANGO YA MAENDELEO YA BAADAE

Mipango ya maendeleo ya baadae ya benki inalenga katika kuboresha utoaji bora wa huduma kwa wateja kuongeza kiwango cha kuwafikia wateja kupitia mtandao wa matawi yake. Malengo maalumu ya benki hadi ifikapo tarehe 31 Desemba, 2014 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza mtaji kufikia shilingi bilioni 18.05 kufikia taraehe 31 Desemba, 2014 ikiwa ni ongezeko la asilimia 45% kutoka shilingi bilioni 11.01 iliyopatikana mwaka 2013. Hii ni kuendana na matakwa ya Benki Kuu inayozitaka benki zote za biashara nchini kuwa na mtaji wa shilingi bilioni 15 ifikapo Machi, 2015

(ii) na kufungua matawi mawili;

(iii) kuanzisha wakala wa huduma za benki mwaka 2014.

(iv) Kuimarisha shughuli za ukopeshaji wa mikopo midogo midogo kwa makampuni hadi kufikia shilingi bilioni 3.11

(v) Kuimarisha shughuli za ukopeshaji wa mikopo mikubwa kwa makampuni hadi kufikia shilingi bilioni 38.98

(vi) Kuendelea kutoa mikopo ya wafanyakazi wenye mishahara inayopitia benki hadi kufikia shilingi bilioni 10.99

(vii) Kuongeza ukusanyaji wa amana za wateja hadi kufikia shilingi bilioni 72.56

(viii) Kufikia kiwango cha urejeshaji mikopo kwa kiasi cha asilimia isiyopungua 97 katika kipindi chote;

(ix) Kuongeza kiwango cha rasilimali za benki hadi kufikia shilingi bilioni 90.63

## 5.16 RASILIMALI WATU

Benki ina wafanyakazi wa kutosha wenye uwezo na uzoefu wa kutosha katika nafasi zote muhimu.

## 5.17 VIHATARISHI

Kadiri benki inavyoendelea kukuza uendeshaji wake inahakikisha kwamba hali hatarishi inadhibitiwa kwa mujibu wa sera na taratibu zote zilizowekwa. Shughuli za kibenki zinazoweza kuwekwa katika hali hatarishi zinazojumuisha shughuli za mikopo, hali ya ukwasi, athari za masoko na athari za kisera. Masuala yote yahusuyo usimamizi wa hali hatarishi yameainishwa na Bodi ya Wakurugenzi kwenye sera za benki ambazo zinatekelezwa na Menejimenti ya benki. Sera hizi zinahusisha uchambuzi, uthamini, ukubalifu na usimamizi wa viwango vya hali hatarishi au muunganiko wa hali hatarishi kwa ujumla wake.Maelezo zaidi ya hali hatarishi inayozikumba benki yameainishwa kwenye kielelezo namba 3 kwenye taarifa ya fedha.

## 5.18 UWIANO WA VIGEZO MUHIMU VYA UTENDAJI

Uwiano wa vigezo muhimu vya uendeshaji wa benki vinavyopima ufanisi wa huduma za benki ulikuwa kama ifuatavyo:

| Vigezo vya uwiano | Maana na uchambuzi wake | 2013 | 2012 |
|---|---|---|---|
| Pato kutokana na | Pato halisi/Mtaji wote mtaji | 3.00% | -7.60% |
| Pato litokanalo na | Pato halisi /Rasilimali zote rasilimali | 0.50% | -1.80% |
| Uwiano wa gharama za pato | Gharama za uendeshaji/ pato halisi | 93.90% | 119.40% |
| Riba kwa rasilimali zinazozalisha | Jumla ya pato litokanalo na riba/(riba itokanayo na amana za Serikali + Salio kwenye benki zingine + mikopo ya benki +uwekezaji kwenye amana nyingine + mikopo yote) | 14.50% | 14.30% |
| Mapato yasiyotokana na riba kwa mapato yote | Mapato yasiyotokana na riba /Mapato yote | 10.10% | 11.50% |
| Mapato kwa kila hisa | Mapato halisi / idadi ya hisa zilizolipwa | 1.10% | -6.50% |
| Mikopo yote kwa wateja wenye amana | Mikopo yote kwa wateja wenye amana/Jumla ya amana | 58.70% | 59.80% |
| Mikopo isiyorejeshwa kwa mikopo yote | Mikopo isiyorejeshwa /Mikopo yeto na karadha | 2.70% | 3.00% |
| Rasilimali zinazozalisha kwa rasilimali zote. | Rasilimali zinazozalisha /Rasilimali zote. | 81.00% | 79.30% |
| Kukua kwa rasilimali zote | Mwelekeo (jumla ya rasilimali za mwaka 2013– Jumla ya rasilimali za mwaka 2012 | 59.90% | 19.40% |
| Kukua kwa mikopo na karadha kwa wateja wenye amana | Mwlekeo (Jumla ya mikopo yote kwa mwaka 2013 - Jumla ya mikopo yote kwa mwaka 2012 | 73.10% | 44.50% |
| Kukua kwa amana | Mwelekeo (jumla ya amana zote kwa mwaka 2013 – Jumla ya amana zote kwa mwaka 2012 ) | 75.90% | 29.10% |
| **HALI YA MTAJI** | | | |
| Mtaji timilifu ngazi ya 1 | Rasilimali zilizohatarishi pamoja na taarifa ya fedha nje ya mizania /Mtaji halisi | 23.120% | 33.76% |

## 5.19 USIMAMIZI WA HALI HATARISHI NA UDHIBITI WA NDANI

Bodi ya Wakurugenzi inazingatia uwajibikaji wake wa mwisho wa kusimamia hali hatarishi na kuhakikisha panakuwepo mfumo wa udhibiti wa ndani kwa ajili ya utendaji bora na kuhifadhi mali za benki. Ni jukumu la Bodi kuhakikisha kuwa mifumo dhabiti na endelevu ya udhibiti wa fedha na utendaji inatengenezwa, kuhakikiwa na kubadilishwa kila inapobidi ili kuhakikisha yafuatayo yanatekelezwa:-

- Uendeshaji kwa ufanisi na tija wa shughuli za kibenki;
- Kulinda mali za benki;
- Kuzingatia sheria husika na taratibu za uendeshaji wa benki;
- Kuhakikisha usahihi wa vitabu vya hesabu na kumbukumbu za miamala ya fedha za benki;
- Kuhakikisha uendelevu wa shughuli za benki katika mazingira ama ya kawaida au hatarishi ; na
- Kuwa na tabia ya uwajibikaji kwa wadau wote wa benki.

